PARADIGMS SCHOOLS

RISALA YA MAHAFALI YA NNE YA KIDATO CHA NNE 2011 KWA MGENI RASMI – Mh MAKONGORO MAHANGA (MB), NAIBU WAZIRI- KAZI NA VIJANA
TAREHE 10/09/2011

Utangulizi:-
Ndugu Mgeni rasmi, Mlezi wa shule ya sekondari, mkurugenzi wa shule za Paradigms, wazazi, wageni waalikwa, waalimu, wanafunzi, mabibi na mabwana, itifaki imezingatiwa, HABARI ZA ASUBUHI

Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyeezi Mungu ambaye kwa Mapenzi Yake Ametupa uhai na kutuwezesha kuwepo mahali hapa.

Aidha napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa mgeni rasmi kwa kukubali kujumuika nasi leo katika sherehe za mahafali ya 4 wanafunzi wetu wa kidato cha nne ,na ya 3 ya darasa la saba na darasa la awali 2011. Tunasema ahsante sana na karibu sana Paradigms.

Ndugu mgeni rasmi, Shule za Paradigms ni shule zinazotoa elimu ya awali, msingi, sekondari kuanzia kidato cha kwanza hadi cha sita, Chuo cha Ualimu ambapo tunatoa kozi za mafunzo ya ualimu wa shule za awali, shule za msingi (GRADE III A) na stashahada ya ualimu (Diploma in Education) pamoja na chuo cha COMPUTER ambapo tunatoa kozi za vyeti na stashada za Tekinohama (ICT). Shule hizi zipo chini ya kampuni ya uendelezaji elimu iitwayo Paradigms Institute Ltd.

Shule hizi zinapokea na kusomesha wavulana na wasichana', wa kutwa na bweni na tunatoa huduma iliyobuniwa na kuratibiwa vizuri kuwaridhisha wateja wa makundi mbalimbali. Tunafundisha masomo kulingana na mitaala ya Taasisi ya Elimu ya Taifa (Tanzania Institute of Education) inayosimamiwa na kutahiniwa na Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA) kwa kutumia lugha ya kiingereza isipokuwa somo la Kiswahili.

Ndugu mgeni rasmi, kuwepo kwa shule zetu nje ya mji, ukubwa wa eneo la shule na mchanganyiko wa shule 4, kumetengeneza mazingira murua ya kufundisha na kujisomea.

Ndugu mgeni rasmi, shule za Paradigms zimeanza kwa nyakati tofauti, kama ifuatavyo:- Februari 2007, shule ya sekondari ilianza kwa wanafunzi wa kidato cha kwanza hadi cha tano, Januari 2008, shule ya awali na msingi ilianzishwa kwa darasa la kwanza mpaka la Sita , Julai 2009, chuo cha ualimu kilianzishwa na Julai 2011, tulifungua chuo cha COMPUTER. Shule zote hizi zimesajiliwa na zinaendeshwa kwa taratibu sahihi zilizowekwa na Taifa na kusimamiwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

TAALUMA

Ndugu mgeni rasmi, taaluma ndilo lengo letu la msingi la kuwepo hapa. Kama tulivyoeleza hapo juu, shule zetu zina umri wa Kati ya miezi 3 mpaka miaka 4.5. Mzunguko wa elimu ni baina ya miaka 2 mpaka 7. Ili kuandaa na kutekeleza mkakati unaopimika unahitajika kutumikia mizunguko 2 au zaidi. Ndio kwanza tunamalizia mzunguko wa kwanza na hivyo tuko katika kipindi Cha tathmini ya mafanikio na changamoto za Mzunguko wa kwanza ili tuweze kujipanga vizuri kwa kukabiliana nazo kwa mikakati sahihi. Mifano ifuatayo inaelezea fursa na vikwazo tulivyokuwa navyo. Shule ya msingi ilianza 2008 ikiwa na wanafunzi 8 wa darasa la kwanza. Kwa sasa wanafunzi hao wako darasa la 4. Hata hivyo utashangaa kuwa zao letu la kwanza la darasa la Saba lilikuwa 2009, 2010 na 2011. Hii ina maana kuwa tulilazimika kupokea wanafunzi wa darasa la 6 toka shule mbali mbali zikiwemo zile zinazotumia lugha ya Kiswahili na tukaweza kuwaandaa kwa muda mfupi na wakafaulu. Kadhalika shule yetu ya sekondari ilianza mwaka 2007 na ikaanza kutoa matunda ya kidato cha nne 2008, mwaka 2008,2009,2010 wakati kundi la kwanza lilitakiwa litoke 2010. Hii ina maana kuwa tulipokea wanafunzi waliokuwa wanasoma katika shule nyingine na tukawaandaa kwa kipindi kifupi kabla ya kufanya mitihani yao. Uzoefu tulioupata umetupa nafasi ya kuandaa mikakati sahihi ya kutuwezesha kusonga mbele kwa uhakika na kwa kujiamini.

Ndugu mgeni rasmi, shule za Paradigms zimekuwa na mafanikio mbalimbali katika nyanja za kitaaluma toka zilipoanzishwa hadi leo. Miongoni mwa mafanikio hayo ni pamoja na:

Kuweza kuongeza kiwango cha ufaulu kwa 70% kwa madarasa yote kuanzia kidato cha kwanza hadi cha sita. Hilo limejihiridhisha katika matokeo yetu ya kidato cha nne na sita ya mitihani ya taifa kwa mwaka 2009 na 2010. Kwa mfano, matokeo ya kidato cha nne ya mwaka jana(2010) tulifanikiwa kufuta divisheni ziro ikizingatiwa kwamba mwaka huo wanafunzi wengi walifeli sana.Kwa kidato cha sita 90% ya watahiniwa wa mwaka 2010 wamefanikiwa kuendelea na elimu ya juu.

Ndugu mgeni rasmi, ikumbukwe kwamba wanafunzi hawa tuliwapokea wakiwa katika hali mbaya sana kitaaluma, lakini tulifanya juhudi kubwa kuwasaidia katika kipindi kifupi tulichokaa nao. Matokeo ya juhudi hizo ni ya kujivunia, kwani ni kazi iliyofanyika kwa muda mfupi sana.

Kwa mwaka huu 2011 wanafunzi 30 walihitimu kidato cha sita, wanafunzi 9 kati yao walisoma kidato cha tano huku wanarudia mitihani ya kidato cha IV ili waweze kupata sifa za kufanya mtihani wa kidato cha sita. Wanafunzi hawa walifanikiwa kupata sifa hizo zilizowawezesha kufanya mtihani wa kidato cha sita na wote walifaulu na 75% yao wamepata nafasi ya kuendelea na elimu ya juu katika vyuo vikuu mbali mbali ndani na nje ya nchi.

Tunajivunia matokeo haya kwani yanatokana na juhudi na kazi nzuri iliyofanywa na timu ya waalimu wetu.

Ndugu mgeni rasmi, katika kuonyesha kweli tumejipanga katika kujiimarisha katika kutoa elimu bora, tumefanikiwa kutoa mafunzo mbalimbali kwa waalimu wetu wa ndani ili kuendana na mabadiliko ya mitaala na kuweza kuboresha huduma zetu zaidi. Kwa mfano; mwanzoni mwa mwaka huu tulitoa mafunzo ya jinsi ya kumuhudumia mteja tukiamini kwamba mteja ndio shina la kufanikinikisha adhima na lengo la serikali na taasisi yetu katika utoaji elimu bora.

Pia kutokana na mabadiliko ya mitaala mara kwa mara tumefanikiwa kuwaendeleza waalimu kupitia mafunzo mbalimbali ya kujifunza na ufundishaji ambayo ni mafunzo elekezi ya jinsi ya kutunga mitihani kuendana na mtaala mpya, kusaisha mitihani pamoja na mbinu mpya zinazomshirikisha mwanafunzi katika kujifunza kama inavyoelekezwa katika mtaala mpya.

Ndugu mgeni rasmi, mwaka huu tunao wanafunzi 48 wanaohitimu kidato cha nne, 17 darasa la saba. Asilimia 75 kati ya wanafunzi hao walihamia shuleni kwetu katika vidato na madarasa mbali mbali. Kadhalika tunao wanafunzi 14 wanaomaliza shule ya awali. Hawa wote tumewaandaa, tumewapima na tunaimani kuwa zao la mwaka huu litakuwa bora zaidi ya lile la mwaka jana.

Ndugu mgeni rasmi, katika ngazi ya shule ya msingi, tumekuwa na mafanikio makubwa sana katika kuhakikisha tunafikia kilele cha mafanikio. Kwa mfano maendeleo ya kitaaluma yamekuwa yakipanda mwaka hadi mwaka kuanzia 2009 hadi sasa. Kipimo cha ukuaji huu wa kitaaluma umepimwa kulinganisha na shule nyingine katika ngazi ya wilaya,mkoa na kitaifa. Kwa mfano zifuatazo ni takwimu zinazoonyesha kiwango cha kukua kwa ufaulu wetu katika shule ya msingi;

Mwaka 2009-shule yetu ya msingi ilikuwa nafasi ya 31 kiwilaya kati ya shule 74, nafasi ya 185 kimkoa kati ya shule 407, na kitaifa nafasi ya 2205 kati ya 14376 wakat Mwaka 2010, shule yetu ilikuwa ya 19 kiwilaya kati ya shule 82, kimkoa shule ilikuwa nafasi ya 60 kati ya shule 433 na kitaifa shule ilkuwa nafasi ya 646 kati ya 14759.

Ndugu mgeni rasmi, kutokana na data hizo inaonyesha ni jinsi gani maendeleo ya shule yetu yamekuwa yakikua kila mwaka. Na kwa mwaka huu tunategemea kupanda zaidi katika kiwango cha kufaulisha na kufikia kiwango cha juu zaidi kitaifa. Mkakati wetu ni kuwa 10 bora kiwilaya kabla ya 2013 na 10

Bora kitaifa ifikapo 2015. Tumedhamiria, tumejipanga, tumefanya mabadiliko makubwa ya kiutendaji na kiusimamizi na tuna imani kuwa tutashinda

Mkakati wetu ni kuendelea kuboresha huduma zetu kitaaluma na kinidhamu mpaka tutakapokuwa mfano bora wa kuigwa – a model school – yaani Paradigm. Njia tupitayo ni nyembamba na ngumu, hata hivyo dhamira yetu ni kubwa na tunaamini kuwa hakuna kitakachotuzuia.

Ndugu mgeni rasmi, katika kuboresha taaluma wanafunzi wetu wa shule zote nne wana nafasi ya kusoma somo la kompyuta ambapo kwa kufahamu matumizi ya kompyuta ni rahisi kwa wao (wanafunzi) kuweza kutumia kompyuta katika zoezi zima la kufundishwa na kujifunza. Tunayo maabara ya kisasa ya tekinohama (ICT) iliyounganishwa na mfumo huru wa mtandao (wireless internet connection) kiasi cha kumwezesha kila mwanafunzi kuwasiliana na ulimwengu kupitia njia ya mtandao kwa urahisi zaidi.Tumelazimika kusisitiza na kuhimiza

somo hili kwa kutambua ukweli kuwa maisha yetu sasa yanategemea tekinohama.

Ndugu mgeni rasmi, kukua kwetu kitaaluma kumejengwa na kuwezeshwa na dhamira ya wakurugenzi, bodi ya shule na wadau mbali mbali kwa kutuwezesha kupata rasilimali sahihi za kuendeshea shule zikiwemo; madarasa, maabara, maktaba, vifaa na kemikali vinavyokidhi haja ya sasa na wakati ujao.

Ndugu mgeni rasmi, Pamoja na kwamba kuna mambo mengi yanayochangia matokeo ya Taaluma kuwa mazuri au mabaya; ufundishaji, usimamizi na ufuatiliaji wa karibu ni mkakati sahihi unaopaswa kuratibiwa na kuhakikiwa kwa umakini mkubwa. Ili kufikia lengo hilo, tumelazimika kuwa na mikakati mingi na endelevu. Sehemu ya mikakati hiyo ni; kuwapima wanafunzi wanapojiunga nasi kujua uwezo wao, kuwapima kila mwezi kujua tija ya utendaji wetu na juhudi zao, kuwachuja kila mwaka kabla hawajajiunga na kidato kinachofuata. Tumeandaa utaratibu maalum wa kuwafuatilia kwa ukaribu waalimu wetu kuona kama wanafundisha kwa umahiri na ukamilifu. Ili kujihakikishia kuwa hatufanyi makosa, tumenunua na kufunga kamera, CCTV CAMERAS madarsani na SERVER yenye uwezo wa kuhifadhi matukio yetu kwa siku 90. Utaratibu huu umekuza ari ya utendaji, na tayari waalimu 4 waliokwazwa na utaratibu huu wameshakimbia kazi. Tunawaomba wateja wetu watuelewe, washirikiane nasi na watuvumilie.

NIDHAMU

Ndugu mgeni rasmi, nina imani kabisa kuwa wewe utakuwa shahidi yangu mbele ya umati huu wa wazazi pamoja na wanafunzi ya kwamba “Hakuna Elimu bila Nidhamu”.

Changamoto za nidhamu kwa wanafunzi zinakuwa siku hadi siku, wanafunzi wanadai demokrasia na uhuru zaidi. Wazazi wanadai malezi na kusikiliza zaidi (mteja ni mfalme) na sisi tumedhamiria kuwa kituo cha malezi bora na elimu iliyotukuka.

Ndugu mgeni rasmi, changamoto iliyopo ni tafsiri ya haki na wajibu baina ya waalimu, wazazi, wanafunzi na jamii. Mkanganyiko huu wa tafsiri ukienda sambamba na umri wa vijana wetu na athari za dunia kuwa kijiji (globalization) vimekuwa vikwazo vikubwa sana katika kufikia malengo yetu ya kukuza nidhamu. Taasisi imejipanga na imechukua hatua mahsusi kuona kuwa tunajenga familia yenye nidhamu na inayofuata maadili na miiko ya Taifa letu.

Ndugu mgeni rasmi, tunaomba wizara, wazazi, jamii na taifa kwa ujumla tujipange upya kuangalia mihimili ya utamaduni wetu, na kutafuta mbinu muafaka za kuwekeza katika nidhamu za watoto wetu. Tukijipanga vizuri na kushirikiana shule zitabaki kuwa vituo vikuu vya malezi na utamaduni wa Taifa letu.

Ndugu mgeni rasmi, katika kupambana na changamoto hizi tumefanikiwa kuunda kamati ya nidhamu pamoja na ushauri nasaha ambapo imekuwa na kazi ngumu ya kuwarudi wanafunzi ili wafuate maadili na tamaduni zetu.

Pia tunakutana na wazazi wa wanafunzi wanaoonyesha kiwango kikubwa cha utovu wa nidhamu na kujadili kwa pamoja makosa aliyotenda mwanae

(mwanafunzi). Tumeunda kamati ya wazazi ya ushauri ili kuhakikisha utawala bora na uwazi katika utekelezaji wa majukumu yetu.

MOTISHA

Kumiliki na kuendesha shule ni changamoto inayohitaji kuangaliwa kutumia tundu la 3 (the third dimension) na kwa umakini mkubwa. Lazima kutambua kuwa kuna wadau zaidi ya 8 wenye maslahi na shule. Kinachotatiza zaidi ni kuwa, sio tu kuwa wana maslahi na shule, bali pia wana maslahi yao binafsi yanayokinzana na yale ya shule. Kazi kubwa tuliyonayo ni namna ya kutambua maslahi yao na kujipanga kuyakidhi bila kuathiri yale ya taasisi.

Tumejipanga na tunatoa motisha zifuatazo kwa wadau wetu.

- ►nyumba kwa waalimu; waalimu 10 kati ya 25 wanaishi katika nyumba za shule.
- ►mikopo midogo midogo; wafanyakazi wanakopeshwa mishahara 2 kukidhi mahitaji yao tunapokuwa na uwezo.
- ►ajira; wanafunzi wetu wanaomaliza na kufaulu vizuri wanaajiriwa na taasisi yetu
- ►masomo kazini; waalimu wanaofanya kazi zao vizuri hupata fursa ya kuendelezwa katika ngazi inayofuata.
- ►wanafunzi wanaofaulu vizuri hupongezwa kwa njia mbali mbali ikiwa ni pamoja na safari za kutembelea maeneo ya kihistoria.
- ► waalimu wanaoshindwa kutimiza wajibu wao vizuri huachishwa kazi
- ► wanafunzi wasiokuwa na nidhamu huachishwa shule

CHANGAMOTO

Shule zetu zinakabiliwa na changamoto kadhaa zinazokwaza ufanisi. Baadhi yake ni hizi zifuatazo:-

A. CHANGAMOTO ZA KITAASISI

1. MAJI

Shule zetu zinavyo visima 3 vinavyotoa maji ardhini ya kutosheleza shule. Hata hivyo maji haya yana chumvi. Upatikanaji wa maji yasiyokuwa na chumvi na ya kutosheleza, ni ama kutegemea Dawasa / Dawasco au kuvuna maji ya mvua au vyote kwa pamoja, Kunahitajika kujengwa matanki yenye ujazo usiopungua gallon 250 m kwa ajili ya kutosheleza matumizi ya sasa na baadae angalau kwa siku 100.Mradi huu unahitaji uwekezaji wa Tshs 86 m.

2 . UMEME

Ndugu mgeni rasmi, tatizo la umeme limekuwa ni kikwazo kikubwa katika kufikia lengo la kutoa huduma na kuipata huduma hiyo kwa ujumla. Hii ni changamoto kwa maana kwamba utoaji wa elimu katika shule yetu unategemea zaidi kujifunza na kufundisha kwa kutumia vifaa vingi vinavyotumia umeme kwa mfano, matumizi projector kufundishia, kuwashia kamera za usimamizi, kufundishia computer na huduma za masomo kupitia mtandao, mwanga kwa ajili ya kujisomea usiku, Tunaomba utufikishie kilio chetu serikalini ili kama ni lazima kufanya mgawo waangalie maeneo ya shule Kama inavyofanyika katika kambi za jeshi na chuo kikuu cha Dar Es Salaam.

3. MICHEZO

Pamoja na kuwa tunavyo viwanja / maeneo ya michezo makubwa kuliko shule yeyote katika wilaya yetu , tunapaswa kuwekeza kikamilifu katika ujenzi na kuendeleza viwanja hivi pamoja na vifaa ili kuboresha na kuendeleza michezo hapa shuleni. Ni imani yetu kuwa wizara yako itatusaidia kupata mfadhili au mbinu za kuwekeza katika eneo hili la michezo.

B.CHANGAMOTO ZA JUMLA

Ndugu mgeni rasmi, pamoja na mafanikio tuliyoeleza juu, bado taasisi yetu, na nyingine zinazotoa elimu nchini, tunakabiliwa na changamoto nyingi. Baadhi yake ni hizi zifuatazo.

(a) Riba:-

Uwekezaji katika elimu unahitaji mtaji mkubwa sana; Sisi kwa mfano tumeshawekeza zaidi ya bilioni moja, 50% ikiwa ni mikopo toka benki mbalimbali na tumeomba zaidi ya sh. 1.3 bilioni kwa ajili ya kuboresha huduma zetu mwakani. Tunategemea kuwekeza bilioni 10 ifikapo mwaka 2017; Fedha zote hizi zinatozwa riba ya 20% - 24% kwa mwaka.

Ni ukweli usiofichika kwamba haiwezekani kuboresha elimu nchini kwa riba za namna hii. Tunaomba na tunashauri serikali ianzishe mfuko au benki maalumu ya uwekezaji katika huduma ya elimu itakayotoza riba isiyozidi 5%; Katika hili ifahamike kuwa riba isipopungua hatimaye mteja ndiye atakayelipia riba na matokeo yake ada zitaendelea kupanda na Watanzania wengi watakosa nafasi za masomo kwani si rahisi serikali iweze kumudu kutoa huduma hii peke yake.

(b) Kodi za majengo:

Ndugu mgeni rasmi, kazi ya kujenga na kuendesha shule za msingi na sekondari ni halmashauri za mji, manispaa na jiji. Halmashauri hizi hupaswa kutoza kodi Mbali toka kwa wakazi wake ili ziweze kutimiza jukumu hili. Wale waliotozwa kodi walipaswa kupatiwa haki ya elimu watoto wao kutokana na kodi hizo. Bahati mbaya Halmashauri hizo zimeshindwa kujenga shule za kutosha kusomesha watoto hawa. Ni kwa misingi hiyo ndio maana taasisi na watu binafsi wameamua kujenga shule za binafsi kuzisaidia Halmashauri kutimiza wajibu wao. Kama halmashauri zitaendelea kutoza kodi hizi (mfano property tax) na serikali kuu ikiendelea kutoza (income tax) ni kuwatoza wananchi wake kodi mara mbili kwani hatimaye kodi hizo zitaingizwa kwenye ada, hivyo tunapendekeza kuwa shule zote zisitozwe kodi ya majengo wala ya mapato ili ziwe na uwezo wa kuboresha huduma na kuzitoa kwa gharama nafuu.

(c) Sheria na kanuni za elimu:

Ndugu mgeni rasmi, sheria na kanuni zinazosimamia elimu ni kali sana na yawezekana dhamira yake ni njema kwa manufaa ya Taifa letu tukufu la Tanzania. Hata hivyo kwa namna zilivyo zinakwaza na kuchelewesha walengwa kufikia malengo yao kielimu. Tunadhani tunachopaswa kufanya ni kuandaa kipimo muafaka cha uelewa mwishoni mwa mafunzo. Katika hili, tunapendekeza kanuni zifuatazo ziangaliwe upya.

(i) Kanuni ya kumlazimisha mwanafunzi awe na alama (3 credits) kabla ya kujiunga na kidato cha (V) tano, ibadilishwe na badala yake atakiwe kuwa nazo kabla hajaruhusiwa kufanya mtihani, wa kidato cha sita (VI).

Kanuni inayoelekeza kumlazimisha mwanafunzi anayetaka kujiunga na chuo cha ualimu awe amemaliza shule si zaidi ya miaka mitano nyuma ibadilishwe na badala yake iwe mwaka wowote ili kumpa nafasi kila Mtanzania mwenye sifa ya kusomea ualimu asome. Hii italiwezesha Taifa kupata idadi kubwa ya waalimu ili kukidhi haja ya mahitaji makubwa yaliyopo. Changamoto za vyeti vya miaka ya nyuma zitafutiwe namna ya kitaalam ya kukabiliana nazo.

Kurudia darasa. Lazima tufanye maamuzi magumu katika masuala nyeti. Inatupasa kuamua kama shule ni taasisi za makuzi au elimu. Inatupasa kuamua kama kipimo cha elimu kinapaswa kufanywa mwishoni au muda wote. Tunapaswa kuamua ikiwa ni busara kuendelea mbele na mwanafunzi mwenye uwezo mdogo hata kama tunajua kuwa hatimaye hatafaulu ama tumsubirishe mpaka aive. Hivi tunapomlazimiza mwanafunzi ambaye mlezi wake yuko tayari kumlipia Ada ya kurudia tunafanya hivyo kwa maslahi ya nani? Inashauriwa kuwa tufufue utaratibu wa kuwapima wanafunzi kila mwaka, wale wasiofikia viwango walazimishwe kurudia mwaka, hasa kama wadhamini wao watakubali kuwalipia ada ya kurudia.

Mabadiliko ya mitaala. Ubadilishaji wa mitaala ni jambo jema likifanywa kwa umakini. Kwa bahati mbaya sana, ubadilishaji wa mitaala yetu umekuwa ukifanywa bila maandalizi ya kutosha na hivyo kuwachanganya wadau na kutokuleta tija inayokusudiwa. Tunaomba wale wanaoamua kubadilisha mitaala watambue kuwa kunahitajika uwekezaji mkubwa katika mafunzo kwa waalimu na wakufunzi. Lazima uwekezaji huu ufanywe wakati muafaka na kwa maslahi ya wadau wote.

Taarifa za maeneleo ya mwanafunzi kitaaluma. Kuna tetesi kuwa kumekuwa na mkanaganyiko mkubwa wa uandaaji wa taarifa hizi kiasi cha kuwafanya watumiaji ama kuhoji uhalali wake na hata kuamua kutozitumia kabisa. Kama tetesi hizi zina ukweli, yatupasa kuliangalia kwa makini kwa kuwa, hatuwezi kuharibu mizani na tukaendelea kujidai kuwa sie ni wapimaji wazuri. Mizania mbovu lazima itoe majibu mabovu.

Upungufu wa waalimu wa III A na Diploma: Ndugu mgeni rasmi, inakisiwa kuwa wastani wa waalimu dhidi ya wanafunzi katika shule za sekonari 1:75 wakati ile wa shule za msingi unakaribia 1:85. Kwa sasa serikali ina uwezo wa kusomesha 2% kwa mwaka. Kwa utaratibu huu tutafikia lengo la 1:40 miaka 50 ijayo. Kama serikali ikiamua kuwalipia AMA kuwakopesha wanaosomea Daraja la IIIA na Diploma, sekta binafsi inaweza kuzalisha waalimu 500, 000 kwa mwaka na kulimaliza tatizo la waalimu ndani ya miaka 5 ijayo. Tunashauri yafanyike maamuzi magumu.

HITIMISHO:

Ndugu mgeni rasmi, tunakufahamu wewe, marafiki zako na uwezo wako. Tunaifahamu nafasi yako katika jamii na heshima uliyojijengea katika kuhudumia watu. Ni imani yetu kuwa, utapata fursa ya kuipitia risala hii kwa umakini na kushirikiana nasi kutafuta ufumbuzi wa changamoto zinazotukabili.

Nashukuru kwa kunisikiliza.